

HALMASHAURI YA WILAYA YA MLIMBA

SHULE YA SEKONDARI MOFU.

mofusecschool@gmail.com
0713476028
Kumb Na. ED/ MOF/SS/F 1 SEL 2020

S. L. P 348
IFAKARA
15 Desemba 2020

JINA LA MWANAFUNZI _____

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MOFU.**

1.0 Utangulizi

Ninayo furaha kukufahamisha kwamba umechaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari Mofu katika kidato cha kwanza mwaka 2021.

Nakupongeza sana kwa kuchaguliwa kujiunga na Elimu ya Sekondari, ni matumaini yangu kwamba utaitumia nafasi hii vizuri.

Shule itafunguliwa tarehe **11 Januari 2021**, na unapaswa ufike shuleni siku hiyo saa 1.00 asubuhi.

Mwisho wa kuripoti Shuleni ni tarehe **22 Januari 2021**. Iwapo kama hujaripoti mpaka siku hiyo, nafasi yako atapewa mwanafunzi mwingine mwenye kiu ya kupata elimu, na wewe pamoja na mzazi wako kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Iwapo kama mzazi wako ameamua kukupeleka Shule ya watu binafsi anapaswa kuja kutoa taarifa Shuleni ikiwa ni pamoja na barua ya uthibitisho wa kupokelewa kwenye Shule husika.

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 SARE ZA SHULE

(a) Sare ya Wavulana

- Suruali mbili za rangi ya damu ya mzee, sampuli ya kitambaa inapatikana kwa mafundi chereheani maeneo ya lhenga na Mofu.
 - Iwe na Malinda (Celebrations 2 kila upande), isiyo na malinda haikubaliki
 - Isiwe Suruali ya kubana, au kubwa sana, iwe Suruali ya heshima
 - Mshono wa Jeans haukubaliki
 - Isiwe na mifuko ya kubandika
 - Iwe na mifuko mitatu, mbele miwili na nyuma mmoja.
- (i) Mashati mawili meupe tetroni ya mikono mifupi yasiwe ya kubana au makubwa sana, yawe na uwezekano wa kuchomekea.
- (ii) Viatu vya ngozi vyeusi vyenye gidamu (vyenye kamba), mabuti na viatu visivyo na gidamu havikubaliki.

(iii) Mkanda wa ngozi rangi nyeusi.

(iv) Soksi rangi nyeusi.

(b) Sare ya Wasichana

- Sketi mbili za rangi ya damu ya mzee, sampuli ya kitambaa inapatikana kwa mafundi chereheani maeneo ya lhenga na Mofu.
- Mshono ni Linda Box.
- Sketi ivuke magoti, sketi fupi haikubaliki. Isiwe Sketi ya kubana.
- **Wanaovaa Hijabu** wanatakiwa kushona nusu kanzu na kitambaa kinachofanana na shati la shule pamoja na sketi ndefu. Iwapo kama hujaelewa mpigie Mkuu wa Shule.

(ii) Mashati mawili meupe tetroni ya mikono mifupi yasiwe ya kubana au makubwa sana, yawe na uwezekano wa kuchomekea.

(iii) Viatu vya ngozi vyeusi vyenye gidamu (vyenye kamba), mabuti na viatu visivyo na gidamu havikubaliki.

(iv) Soksi rangi nyeupe

(c) Sare za Michezo

Sare za michezo ni , Fulana ya michezo pamoja na **Truck Suit**, raba au viatu vyovyote vinavyofaa kwa ajili ya michezo pamoja na mazoezi ya viungo.

2.2 VIFAA VYA MASOMO

Unatakiwa kuja na daftari za kutosha, Shule yetu ina masomo kumi na moja (12), (Uje na **Counter Books**) pia uje na kalamu na mkebe wa hesabu.

3.0 Sheria na Kanuni Muhimu za Shule hii

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na 25 ya Mwaka 1978 na kama ilivyorekebisha kwa Sheria Na 10 ya Mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi mara baada ya kufika Shuleni.

- (a) Heshima kwa viongozi, wazazi, walimu, Wafanyakazi wote, Wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- (b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya Shule kulingana na ratiba ya Shule ni lazima.
- (c) Kuwa na muda wa kujisomea wakati wa usiku ukiwa nyumbani, na sio kuzurura mitaani.
- (d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine unazopewa.
- (e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya muda wa kuwepo ndani ya mipaka ya shule na muda gani wa kuwepo nje ya mipaka ya Shule
- (f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- (g) Kuvaa sare ya Shule wakati wote unapotakiwa

- (h) Kuzingatia ratiba ya Shule wakati wote
- (i) Kutunza mali ya umma.

4.0 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa Shule mara moja.

- (a) Wizi
- (b) Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocain, mirungi, kubeli n.k
- (c) Kupigana au kumpiga mtu yeyote
- (d) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- (e) Uasherati, ushoga, ubakaji na uzinzi
- (f) Kuoia au kuolewa
- (g) Kudharau Bendera ya Taifa
- (h) Kupata mimba au kutoa mimba, au kusababisha mimba
- (i) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa Shule au watu
- (j) Kukataa adhabu
- (k) Kuwa na simu ya mkononi, ni marufuku mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi popote.

5.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa Shuleni siku ya kuripoti

- (a) Medical Examination Form (Fomu ya hospitali) ambayo itajazwa na Mganga wa Hospitali ya Serikali
- (b) Fomu ya usajili.

Soma vizuri maelekezo haya kama kuna sehemu huielewi uliza kwa piga simu.

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MOFU.

ANGELA O. MKOKO.
Mkuu wa Shule

HALMASHAURI YA WILAYA YA MLIMBA

SHULE YA SEKONDARI MOFU

MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. JINA LA MWANAFUNZI _____

2. TAREHE YA KUZALIWA _____

3. MAHALI ULIPOZALIWA (WILAYA) _____

4. JINA LA MZAZI/MLEZI _____

5. MAHLI UNAKOTOKA (a) KITONGOJI _____ (b) KIJIKI _____

6. SHULE YA MSINGI ULİYOSOMA _____

7. ANUANI YA MZAZI _____

8. MIMI (MWANAFUNZI) _____

NAKUBALI/SIKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MOFU NA KWAMBA
NITAFUATA SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZOTE ZA SHULE

SAINI _____ TAREHE _____

MAELEZO YA MZAZI/MLEZI

1. JINA LA MZAZI/MLEZI _____

2. KAZI UNAYOFANYA _____

3. MAHALI UNAPOISHI SASA KIJIKI NA MTAA _____

4. NAMBA YA SIMU _____

UTHIBITISHO

MIMI _____

MZAZI/MLEZI WA _____

NAAPA KWAMBA MTOTO HUYU NITAMSIMAMIA AWEZE KUSOMA MPAKA ANAMALIZA
SHULE, IWAPO KAMA ATATOROKA AU KUACHA SHULE NICHUKULIWE HATUA KALI ZA
KISHERIA

SAINI _____ TAREHE _____

MLIMBA DISTRICT COUNCIL

MEDICAL CERTIFICATE

MOFU SECONDARY SCHOOL,

P. O. Box 348

IFAKARA

15/12/2020

Simu: 0713476028

To the Medical Officer,

.....
.....

REF:

Please examine the above named student as to her/his physical and mental fitness for being student.

Some of defect will hinder the student for Secondary Schools' Education.

1. a). Eye sight
- b). Hearing
- c). Limbs
- d). Speech
- e). Venereal disease
- f). Leprosy
- g). Epilepsy

2. Neurosis

3. Other serious diseases (name them)

.....
.....
.....

I have examined the above-named student and confirm that she is physically fit/not fit for a full time Secondary School Education.

Name..... Signature Date.....

STATION.....

DESINATION..... N.B.,

(I request this form to be returned to the school in a sealed envelope)